JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

**Mji wa Serikali - Mtumba, Barabara ya Afya, S. L. P 573 - 40478 Dodoma.**
**Simu Na: 255(026)2963341/2963346, Nukushi: 255(026)2963348**
**Barua Pepe: ps@jamii.go.tz, Tovuti: www.jamii.go.tz**

# TAARIFA KWA UMMA

## TAHADHARI YA ATHARI ZA EL NINO KATIKA MVUA ZA VULI ZA MWEZI OKTOBA – DESEMBA, 2026

Tarehe 18 Agosti, 2026 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitoa rasmi utabiri wa msimu wa mvua za vuli (Oktoba – Desemba) 2026, ambao unaathiriwa kwa kiwango kikubwa na hali ya El Nino yenye nguvu kubwa inayotokana na joto la bahari kuwa juu ya wastani katika Bahari ya Pasifiki, hali itakayochagiza ongezeko la mvua za vuli 2026 kuwa za juu ya wastani katika baadhi ya maeneo hapa nchini.

Baadhi ya athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hali hiyo ni pamoja na kutokea kwa mafuriko, maporomoko ya ardhi, kujaa kwa mito na mifereji, uharibifu wa miundombinu ya barabara, reli, madaraja na majengo, uharibifu wa mali na mazao, pamoja na kuongezeka kwa hatari ya magonjwa yanayotokana na matumizi ya maji yasiyo salama. Kufuatia hali hiyo, Wizara inatoa wito kwa:

1. **Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii:**
   Kutoa elimu na tahadhari kwa jamii kuhusu athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mvua za El Nino katika baadhi ya maeneo hapa nchini; kufanya utambuzi wa wananchi walio katika mazingira hatarishi, hususan watoto, wazee, watu wenye ulemavu na kuchukua hatua mapema; pamoja na kufanya maandalizi ya utoaji wa msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa wananachi watakaoathiriwa na mvua za El Nino;

2. **Wazazi, Walezi, Walimu na Jamii kwa Ujumla:**
   Kuchukua tahadhari mapema kwa kufuatilia taarifa rasmi za hali ya hewa; kuepuka kuvuka mito au maeneo yaliyofunikwa na maji; kutoa usaidizi kwa watu wenye ulemavu na wazee wasiojiweza; kutoruhusu watoto au wanafunzi kucheza karibu na mifereji, mitaro, mito, makalavati, madaraja na maeneo ambayo maji yanapita kwa kasi; kusafisha mitaro na mifereji ya kupitisha maji;

kuimarisha makazi yaliyo katika mazingira hatarishi; pamoja na kuhakikisha maji ya kunywa na kupikia yanakuwa salama wakati wote; na

3. **Wakazi Wanaoishi Katika Maeneo Mbalimbali ya Mabondeni**:
   Wakazi wanaoishi katika maeneo ya mabondeni, karibu na mito, pamoja na maeneo yenye historia ya mafuriko au maporomoko ya ardhi wanapaswa kuwa waangalifu zaidi kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini, ikiwemo kuhama mapema katika maeneo hatarishi.

Charles F. Komba
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,**
**WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**
**19 Septemba, 2026**